PORI LA AKIBA LA LITUMBANDYOSI

Siri ya masalia ya mijusi wakongwe duniani





Na Albano Midelo

MIAMBA ya Kusini mwa Tanzania katika Bonde la Ruhuhu mkoani Ruvuma imefichuka siri iliyolala kwa miaka milioni 240.

Ni siri ya masalia ya aina tatu za mijusi wakongwe, wanaohusishwa na chimbuko la viumbe wa kale waliotawala dunia kabla ya 'kuwapo ndoto' ya kuwapo binadamu.

Masalia haya yamegunduliwa katika Pori la Akiba la Litumbandyosi, Bonde la Ruhuhu wilayani Mbinga, Ruvuma na sasa yanaanza kubadili Ruvuma kuwa kitovu kipya cha utalii wa kiakiolojia Afrika Mashariki.

Ugunduzi uliotikisa historia Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anasema masalia hayo yamepatikana katika maeneo ya Manda, Lifua, Kingori na Usili ndani ya bonde lenye historia pana ya mabaki ya viumbe wa kale.

Aina hizo tatu za masalia zimepewa majina ya kitaalamu: Ruhuhuensis aliyegundulika maeneo ya Kingori na Usili mwaka 1950; Ruhuhuaria aliyegundulika Manda na Lifua mwaka 1930 na mgunduzi, Francis Rex Parrington pamoja na Ruhuhucerberus yaliyogunduliwa Kawinga mwaka 2002.

Kwa mujibu wa rekodi za utafiti, mabaki ya Ruhuhuaria ndiyo ya kwanza kugunduliwa mwaka 1930 na Rex Parrington, mwanasayansi Mwingereza aliyefanya uchunguzi wa tabaka za miamba za Lifua–Manda.

Mwaka 1950, masalia ya Ruhuhuensis yaligunduliwa katika mwamba wa Usili, na baadaye mwaka 2002, 'dinosaur' (dinosari) wa Ruhuhucerberus.

Utafiti wa mwisho mkubwa ulifanyika 2007–2008, ukihusisha timu za kimataifa zikiongozwa na Ken Angielczyk na Bill Simpson kutoka Makumbusho ya Historia ya London, Chuo Kikuu cha California, Washington, Uingereza na Marekani.

Wanasayansi wanaamini kuwa viumbe hawa walikuwa na urefu wa meta 2.7 hadi 10, miguu minne kama mamba, shingo ndefu na mkia mrefu.

Aidha, walikuwa sehemu ya kundi la 'archosaurs', kizazi cha mamba na ndege ambacho ndicho chanzo cha dinosari.

Ugunduzi huu umejaza pengo kubwa la kimageuzi katika historia ya dinosari na sasa Bonde la Ruhuhu linaaminika kuwa na rekodi ya dinosari mwenye umri mkubwa kuliko wote kuwahi kugunduliwa duniani.

Tendaguru; ushahidi wa urithi wa Tanzania

Tanzania si mgeni katika historia ya masalia ya viumbe wa kale. Miaka zaidi ya 100 iliyopita (1907–1909), masalia ya dinosari mkubwa anayejulikana kama Tendaguru yalivumbuliwa wilayani Kilwa, mkoani Lindi, wakati wachimbaji madini walipokutana na mabaki yake.

Mabaki hayo yalisafirishwa kwenda Ujerumani na wataalamu, yakaundwa upya, na leo dinosari huyo anasimama kama alama ya urithi wa Tanzania katika Makumbusho ya Berlin tangu mwaka 1889.

Tendaguru ana sifa za kipekee za uzito wa tani 5, kima (urefu kwenda juu) meta 13.7, uzito wa moyo kilo 400 na chakula chake ni mimea (herbivore).

Ingawa Tendaguru ni kivutio kikubwa Ulaya, masalia ya Ruhuhu yanaenda mbali zaidi si kwa ukubwa, bali kwa umri na thamani ya kihistoria inayoweza kuandika upya simulizi la chimbuko la dinosari duniani.

Fursa mpya kiuchumi

Kwa mujibu wa Shirika la Utalii Duniani (UNWTO) mwaka 2025, utalii wa urithi wa kiakiolojia unakua kwa kasi ya asilimia 7.8 kila mwaka na unachangia takribani asilimia 10 ya watalii wote wa kimataifa.





Hii inaifanya sekta hii kuwa lulu mpya ya kimkakati kwa mataifa yanayomiliki masalia ya kipekee.

Kwa Tanzania, sekta ya utalii kwa ujumla ilichangia asilimia 17.2 ya Pato la Taifa (GDP) mwaka 2024.

Kusini mwa Tanzania licha ya kuwa na vivutio vingi, bado inapokea chini ya asilimia 30 ya watalii wote wa ndani na nje ya nchi, hali inayochochea mkakati wa serikali kupanua ukanda huo katika sekta ya utalii.

Challe anaeleza kuwa, masalia ya Ruhuhu yanaweza kuongeza idadi ya wageni Ruvuma kwa asilimia 20 hadi 35 iwapo yatawekewa miundombinu bora ya kutembelea na kutangazwa kimataifa.

Sera, sheria na ulinzi wa urithi

Ugunduzi huu unalindwa na mifumo ya kisheria na kisera, ikiwemo Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999, Toleo la Maboresho 2025.

Sera hiyo inasisitiza kupanua vivutio vya utalii nje ya Ukanda wa Kaskazini na kuendeleza utalii wa urithi na akiolojia Kusini.

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori inatoa ulinzi kwa rasilimali na maeneo ya vivutio vya ndani ya mapori ya akiba.

Kadhalika, Sheria ya Mambo ya Kale inazuia usafirishaji wa masalia ya kihistoria nje ya nchi bila idhini ya serikali na wataalamu wa mamlaka husika.

Mkakati wa Utalii Kusini (Southern Tourism Circuit Initiative) 2022–2030 unalenga kuunganisha mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara katika kutangaza vivutio na kuongeza mapato ya sekta.

Kwa sasa, masalia Bonde la Ruhuhu yamegunduliwa ndani ya Pori la Akiba la Litumbandyosi.

Pori hilo lina ukubwa wa kilometa za eneo 494. Mchakato wa kulifanya pori la wanyamapori ulianza 2003 kwa ushirikiano wa serikali na vijiji vinavyozunguka vikiwemo vya Litumbandyosi, Kingore, Paradiso, Luhagara, Ruanda, Mtunduwalo na Ndongosi.

Bioanuwai ya Litumbandyosi

Mbali na urithi wa akiolojia, pori hilo pia ni hazina ya wanyamapori likiwa sehemu ya ushoroba wa uhamiaji wa wanyama kutoka Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (zamani Selous) kuelekea Hifadhi ya Niassa nchini Msumbiji.

Wanyama wanaopatikana hapa ni pamoja na tembo, chui, kiboko, nyati, faru, pofu, swala, parahala, nyoka adimu, nguruwepori, nyani, kware, kanga, njiwa na zaidi ya aina nyingine 370 za ndege.

Hii inafanya Litumbandyosi kuwa na thamani ya utalii wa wanyamapori na utalii wa akiolojia mchanganyiko unaoweza kufanya Mkoa wa Ruvuma kuwa aina mpya ya utalii kimataifa.

Changamoto huwa hazikosekani

Licha ya kuwapo fursa nyingi, pia kuna changamoto za msingi.

Changamoto hizo ni pamoja na miundombinu ya barabara kufika maeneo ya Manda na Lifua ambayo bado si rafiki sana hasa katika msimu wa mvua.

Aidha, kituo maalumu cha kutunza na kuonesha masalia bado hakijajengwa na uelewa wa jamii kuhusu thamani ya masalia unahitaji kuongezwa.

Ardhi ya Bonde la Ruhuhu imefichua hazina ambayo si tu masalia ya mijusi, bali ushahidi wa mwanzo wa uhai uliobadili dunia.

Huo ni urithi unaoweza kuinua uchumi, kuvutia sayansi ya kimataifa na kuipa Tanzania nafasi ya kipekee katika ramani ya chimbuko la dinosari duniani.

Wakati mataifa mengine yanatafuta historia, Tanzania inaiishi, inaishika na sasa inapaswa kuiuza kwa ulimwengu. Ikiwekeza kimkakati, Bonde la Ruhuhu Ruvuma linaweza kuwa Serengeti ya akiolojia.

Tanzania ya Samia na tuzo ubora wa utalii duniani

Inatoka Uk. 9



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Ashatu Kijaji (wa pili kushoto) akizungumza na watalii walipokuwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi mkoani Morogoro hivi karibuni.

wananchi wa kawaida wakiwemo waongoza watalii, wakulima, wafugaji, wasanii, mama lishe, madereva na wawekezaji wakubwa.

"Ni muhimu tukumbuke jambo moja la msingi kuwa, utalii hauwezi kustawi bila amani, usalama na utawala bora, misingi ambayo Tanzania imeendelea kuilinda kwa nguvu zote," anasema Dk Kijaji.

Fauka ya hayo, anasema sekta ya utalii inaendelea kuimarika kwa kasi kutokana na jitihada za serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha utangazaji wa kimkakati, kuboresha miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, reli, bandari na kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Anasema ili kuimarisha ushindani wa Tanzania kwenye soko la utalii kimataifa, wasimamizi wote wa vituo vya utalii nchini pamoja na wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara hiyo wanapaswa kuhakikisha wanakuja na mazao mapya ya utalii yenye ubunifu.

Ubunifu huo ni tofauti na uliozoeleka na uwe unaoongeza muda wa mtalii kukaa nchini, kuongeza matumizi ya mtalii na kuvutia masoko mapya ya ndani na nje ya nchi.

"Ni wajibu kwa wasimamizi wa hifadhi kuona yale mazao ya utalii ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu yafanyiwe maboresho ya kimkakati ili yawe na mvuto mpya zaidi," anasema Dk Kijaji.

Mikakati ya kuvifanya vivutio hivyo kujulikana na kufikika ni pamoja na kujenga miundombinu mipya na kuboresha iliyopo ili Tanzania iendelee kuwa kivutio cha kipekee, shindani na chenye ubunifu endelevu katika soko la utalii duniani.

"Nihamasishe na kutoa wito kwa Watanzania wote kutenga muda na kuja kutembelea vivutio vyetu, pia taasisi zetu zinazohusika na masuala ya utalii zije na progamu maalumu zitakazowezesha Watanzania wa makundi mbalimbali kutembelea vivutio hivi," anasema.

Anawahimiza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya nchini kushiriki kikamilifu kuhamasisha utalii wa ndani katika maeneo yao, kama ishara ya kumuunga mkono mhifadhi na mwongoza watalii namba moja nchini, Rais Samia.

Kwa mujibu wa Dk Kijaji, hatua hiyo itawezesha kufikia lengo la watalii milioni nane ifikapo mwaka 2030, kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025.

Dk Kijaji anamshukuru Rais Samia kwa utayari na ujasiri wake wa kunyanyua sekta ya maliasili na utalii, jambo lililowezesha Tanzania kupata tuzo tano kubwa zinazohusiana na masuala ya utalii duniani kwa mwaka 2025.

Anazitaja tuzo hizo kuwa ni; 'Kituo Bora Duniani kwa Utalii wa Safari (World's Leading Safari Destination – Tanzania) na 'Serengeti ni Hifadhi Bora Duniani' (World Leading National Park – Serengeti National Park).

Tuzo nyingine ni 'Tanzania ni Kituo Bora cha Utalii Afrika (Africa's Leading Destination – Tanzania), 'Ngorongoro ni Kivutio Bora cha Utalii Afrika (Best Tourist Atraction Ngorongoro) na 'Zanzibar ni Kituo Bora cha Mikutano ya Mashirika na Mapumziko' (African's Best Cooperate Retreat Destination - Zanzibar).

Aidha, Dk Kijaji anasema katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, serikali imewekeza zaidi ya Sh bilioni 284 kuimarisha miundombinu katika maeneo mbalimbali ya hifadhi.

Anaitaja miundombinu hiyo kuwa ni pamoja na viwanja vya ndege, malazi kwa watalii na watumishi, kuboresha malango ya kuingilia wageni na vituo vya kutolea taarifa za watalii katika hifadhi za taifa Ruaha, Mikumi, Nyerere na Udzungwa.

Hivyo, anasema kutokana na jitihada hizo kubwa, Tanzania imeteuliwa kuwa mwenyeji wa tukio la utoaji tuzo za kimataifa kwa ngazi ya dunia zinazoitwa World Travel Awards (WTA) zinazotegemea kufanyika mwishoni mwa mwaka 2026.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Augustine Massesa anasema kujengwa miundombinu ya Reli ya Kisasa (SGR) kumewezesha hifadhi hiyo kuwa wanufaika wakubwa kwa kupata watalii wa ndani na nje.

Kwa mujibu wa Massesa, uwepo uwanja wa ndege ndani ya hifadhi hiyo umeongeza idadi ya watalii sambamba na kuwepo malazi kunakomwezesha mtalii kupata mazingira mazuri ya kufanya utalii ndani ya hifadhi, na wengine kulala kwa sababu miundombinu ni rafiki.

Diwani wa Viti Maalumu, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Madina Fentu ni miongini mwa watalii 100 wa ndani waliotembelea hifadhi hiyo siku ya kuaga mwaka 2025 na kukaribisha mwaka 2026.

Madina anasema kwa kutembelea hifadhi hiyo, amepata elimu kubwa zaidi ya matarajio yake.

"Nilitarajia kuburudika zaidi na si kupatiwa elimu ya kujua utofauti wa tabia za wanyama, mimea na maisha yao kwa ujumla. Nimepata elimu ya historia zao kutoka kwa waongoza watalii; namna wanavyoishi mfano walivyomwona simba na wanyama wengine katika uhalisia wao…" anasema Madina.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima anasema mkoa huo umekuwa kituo kikuu cha utalii wa ndani unaochangiwa na miundombinu ya kisasa, hasa ya barabara na SGR.

Malima anasema miundombinu hiyo rafiki na mingine ikiwamo ya ndani, imewarahisishia watalii wa ndani na nje ufikiaji wa vivutio vya utalii vilivyopo mkoani kwa wakati na kwa urahisi.

Kwa mujibu wa Malima, Mkoa wa Morogoro una vivutio vingi vya utalii vinavyopatikana katika hifadhi za taifa za Mikumi, Udzungwa na Nyerere pamoja na Pori la Akiba la Wami Mbiki linalosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) pamoja na vivutio vingine vingi vikiwamo vya malikale.

"Kwa sasa, mkoa umetangaza nafasi ya uwekezaji katika maeneo ya Doma katika wilaya za Mvomero na Kilosa, hivyo tunaiomba Wizara ya Maliasili na Utalii iyabebe malengo haya na kuyatangaza," anasema.

Mchango wa jamii katika kuimarisha umoja wa kitaifa

Inatoka Uk. 11

Watu wengi hawatambui kuwa maridhiano na umoja si wajibu wa kimaadili pekee, bali pia huleta manufaa makubwa ya kimaendeleo.

Jamii yenye umoja ina uwezo mkubwa wa kushirikiana katika miradi ya kiuchumi, kuvutia uwekezaji na kusimamia rasilimali zilizopo kwa haki.

Umoja hupunguza migogoro inayosababisha kuvurugika kwa shughuli, huendeleza ubunifu na huimarisha nguvu ya pamoja katika majadiliano.

Jamii zinazojenga imani baina yao hukabiliana vyema na changamoto na kupona haraka zaidi baada ya misukosuko.

Kimsingi, elimu ni moja ya zana zenye nguvu zaidi za kukuza umoja na maridhiano.

Kwa mtazamo wangu, shule, vyuo vikuu na programu za elimu ya jamii husaidia kuunda maadili, uvumilivu, fikra makini na utambulisho wa kitaifa.

Elimu ya uraia inahimiza raia kuelewa haki na majukumu yao katika kukuza amani na mshikamano wa kijamii.

Jamii zinapowekeza katika elimu, huunda raia wenye uelewa wanaoweza kupinga mgawanyiko, wanaoshiriki kikamilifu katika utawala na hata wanaochangia maendeleo ya amani.

Ni dhahiri kuwa, vijana wanaotambua umuhimu wa umoja hawako katika hatari kubwa ya kudanganywa au kuingizwa katika itikadi hatari za mgawanyiko.

Hao, hawapotoshwi kirahisi na itikadi za migawanyiko au matumizi mabaya ya kisiasa.

Uongozi imara wa jamii ni muhimu katika kuongoza juhudi za maridhiano na upatanishi. Viongozi wote lazima waige uadilifu, haki, uwazi na ujumuishi.

Uongozi unapokuwa wajibifu na wenye mwitikio, uaminifu katika taasisi za kijamii huongezeka na kupunguza uwezekano wa migogoro.

Hata hivyo, umoja haupaswi kunyamazishwa na kuzuia malalamiko halali.

Maridhiano yanahitaji kusikiliza, kutambua wasiwasi uliopo pamoja na kushughulikia ukosefu wa usawa badala ya kupuuza.

Umoja wa kweli haujengwi kupitia kukandamiza, bali kupitia haki na maendeleo ya pamoja.

Kwa kuwa nimebahatika kupitia maeneo mbalimbali nchini, naweza kuthibitisha kwamba umoja hauwakilishi tu mafanikio ya kihistoria, bali pia ni wajibu endelevu kwa taifa.

Hapa, siku zote jumuiya zinakuwa kiini muhimu cha umoja wa kitaifa.

Kupitia kukuza maridhiano, kushiriki katika mazungumzo jumuishi, kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi na kuunda fursa za maendeleo jumuishi, jamii zina jukumu kubwa kuhifadhi amani na maelewano yanayotambulisha taifa letu.

Kuimarisha umoja si juhudi ya pekee tu; ni harakati inayoendelea inayohitaji huruma, ushirikiano na kujitoa bila kuyumba kwa kila mtu katika jamii.

Jamii zinapochagua maridhiano badala ya mgawanyiko na kuweka kipaumbele katika ushirikiano badala ya migogoro, zinaweka msingi imara zaidi wa utulivu wa kitaifa, ustawi na matarajio ya pamoja kwa manufaa ya vizazi vijavyo.